MWITO PROG 1125 KISWAHILI SCRIPT

SCRIPTURE:ROMANS 7:23-25

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Kwa mara nyingine tena idhaa hii inakuletea kipindi cha Mwito.Ninaamkni kuwa hujambo msikilizaji wangu na kwamba u tayari tena kujumuika name kwa hiki kipindi cha Mwito.Makala ya leo ni nambari 1125.Ninakupatia nambari hiyo ili uweze kujua ni kipindi gani ambacho labda ulikuwa na swali nacho au hukukifahamu vizuri.Kama ilivyo ada nakufahamisha kuwa kipindi hiki kimefadhiliwa na huduma ya Kimataifa ya Macedonian Call chake mchungaji Harold Williams.Katika muda wa dakika 15 zijazo tutasoma pamoja maandiko kutoka kitabu cha Warumi na kufafanua aya kwa ya na sura kwa sura.Lengo la kipindi hiki ni kukushirikisha katika mbnu za uenezaji wa neno la Mungu kwa njia zote Ikiwa ungependa kupokea Biblia baki nami kwa muda huo kwa kuwa nitakueleza jinsi gani unavyoweza kujipatia agano jipya la

Biblia.Ikiwa ndugu msikilizaji hukuwa nani katika kipindi kilichopita nakukumbusha kuwa bado tunachambua maandiko kutoka kitabu cha Warumi.Kwenye kipindi kilichopita tuliangazia aya za 23 hadi 25 ambazo zinafunga sura ya 7 .Hebu tujikumbushe…….***Ole wangu maskini mimi.Ni nani ataniokoa na mwili huu wa mauti? Namshkuru Mungu kwa Yesu Bwana wetu.Basi kama ni hivyo mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu,bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi.***

Karibu ndugu msikilizaji kwa makala ya leo ya kipindi cha Mwito.Jinsi nilivyoelezea kwenye kipindi kilichopita tulifunga sura ya 7 kwenye kipindi kilichopita na sasa leo tutaanza kuangazia aya za kwanza za Warumi sura ya 8.Kuna masimulizi kuwahusu walimu wa neno la MUngu ambao walikuwa wakijadili kuhusu neno la Mungu.Waliulizana ni sura gani nay a kitabu kipi cha Bibilia ambyo ina mvuto mkubwa zaidi.Ni ajabu kwa kuwa 75 ya walimu hao na wasomi maarufu wa neno la Mungu walichagua kitabu cha Warumi .Isitoshe wote walisema sura ya 8 inavutia mno kati ya sura zote za kitabu hicho.Na

huenda ikakushangaza kwamba hata nmi pia nakipenda kitabu hichi cha Warumi,mbali na sura hiyo ya nane.Sina shaka kwamba sura ya nane ya kitabu hicho cha Warumi ni miongoni mwa zile zinazopendwa sana na wasomi na walimu wa neno duniani.Najua wengi wetu pia tungetaja sura ya pili ya kitabu cha Waefeso inayoanza hivi…***Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu ambazo mliziendea zamani kwa kumfwata mfalme wa uwezo wa anga,roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi…..***Na vile vile sura ya 13 ya wakorinthno wa kwanza inayosema…***Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika,kama sina upendo,nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao.*** Hiyo ndiyo sura maarufu kuhusu upendo.Labda nawe unayo sura unayoipenda kutokana na sababu unazozijua weye mwenyewe.Ningependa nieleweke kwamba kwa kusema hivi simaanidshi nyingine hazivutii.Haya ni maoni tu ya wasomi nawe pia una yako.Vyovyote vile Bibilia nzima ina mvuto wake na iliandikwa na watumishi walivyosukumwa na roho mtakatifu wa Bwana.

Nam tukianzia mwanzoni kabisa mimi si msomi ,lakini ninalielewa neno la Mungu na nimelifundisha pia.Lakini bado ni mwanafunzi.Na kartika maisha yangu yote ningali na uhai nitasalia kuwa mwanafunzi kwa kuwa kila kukicha neno la Mungu linajifunua kwangu kwa njia mpya kabisa.Naomba tufungue aya ya kwanza ya sura ya 8 ya Warumi …..***Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika kristo Yesu.Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule uliokatika kristo yesu imeniacha huru,mbali na sheria ya dhambi na mauti.Maana yale yasiyowezekana kwa sheria kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili,Mungu kwa kumtuma mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi na kwa sababu ya dhambi,aliihukumu dhambi katika mwili,ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi tusioenenda kwa kufwata mambo ya mwili,bali mambo ya Roho.***

Somo letu limeanza na maneno…Sasa basi.Je si hiyo ni ajabu.Neno basi lina maana ya kitu ambacho kimewahi kuzungumziwa hapo kabla.Kama tungalitaka kutoa kwa muhtasari mafundisho ya sura zote za nyuma basi tungegusia

tu sura mbili za mwisho yaani sura ya 6 na ya saba.Zote zinazungumzoa kuhusu tatizo kubwa linalokumba wale ambao hasa wameokoka na wangependa kumtumikia Kristo.Hali ya utu wa kale ambao hutuandama na kuturudisha nyuma katika dhambi.Lakini kuna ule utu upya tuliopewa tulipookoka ..ule unaotamani kumtumikia Kristo.Hali ya mvutano iliopo kati ya asili hizo mbili ndiyo imekuwa kiini cha sura hizo mbili na maudhui ya mtume Paulo kuandika kitabu hiki kwa warui ambao walijivunia sana usomi na falsafa za kisomi.Mkanganyo huo ni kizingiti kikubwa kwa wokovu na maisha ya ukristo kwa ujumla.Hebu tuanzie mwanzoni kabisa.Ulipomkaribisha Kristo kuja maishani mwako bila shaka ulifahamu angekusamehe dhambi zako.Uliamini kuwa jinsi maandiko yasemavyo ukiliamini neno lake utaokoka.Na ndivyo ilivyofanyika.Ulisamehewa dhambi zako na kufanyika kiumbe kipya.Ikiwa hukuamini hivyo ,basi hata wokovu ulio nao si wa hakika.Ulikuwa na shaa.Lakini ikiwa ulimwamini Kristo katika moyo wako ulifanyika kiumbe kipya.Sijasema hivyo ,neno la Munbu linasema hivyo.Ikiwa basi uliokolewa ,basi una zile nafsi

mbili.Ile ya zamani na ile mpya.Ni kwamba jukumu lako ni kuilea na kuikuza ile asili ya pili.Ule utu upya uliopatiwa ulipookoka.Ile nafsi inayochukia dhambi.Ile asili mpya haina uharibifu na mbegu yake ilipandwa na Roho mtakatifu na ndilo chimbuko la tumaini la uzima wa milele.

Kwanza kabisa wokovu ni wa nani? Je? Kristo ndiye aliyekuokoka au ulimsaidia katika tendo ilo.Ikiwa alikuokoa na anakudumisha basi sasa ni dhahiri kuwa… ***Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika kristo Yesu.*** Yaani wewe uliyeokoka huna hukumu ya adhabu kwa kuwa uko ndani ya Kristo.Na kwa usemi huo naomba kutamatsha somo la leo ,ili tuendelee kwenye kipindi kijacho.Lakini sijui ikiwa wewe huna hukumu mbele zake ama bado huna uhakika wa maisha ya umilele .Nakuuliza je? Umeshamkabidhi Kristo maidha yako ili uondolewe ile adhabu ya hukumju? Yaani umeokoolewa kwa damu ya Yesu au bado? Ikiwabado chukua fursa bii umkiri na kutubu dhambi zako ili akufanye kiumbe kipya.Nasubiri uchukue hatua hiyo.

Tubu dhambi zako na umkubalie Yesu kuongoza maisha yako.Ukishatubu,tafahadhali mwende mwongofu yeyote anayeamini injili ya wokovu ambaye atakuelekeza kwa kanisa litakalokusaidia kukua kiroho.IKiwa unahudhuria kanisa linaloamini wokovu.Aidha mwende mchungaji wako na umweleze hatua ambayo umechukua naye atakusaidia. unaweza pia kuniandikia au unipigie simu na nitakuelekeza cha kufanya ili uweze kuhifadhi wokovu wako.Na kufikia hapa ndipo natia tamati kipindi hiki cha Mwito nambari 1125.Naomba tukutane katika makala yajayoo.Mwalike rafiki yako ili mkidikilize pamoja kipindi hiki na mtutumie maoni yenu kuhusu jinsi h kukiboresha. Tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Nitumie arafa yako kwa nambari hii -0721 970 520. Au 020 2679842 Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu

kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya kwanza,ya pili na ya 3 ya sura ya 8 ya kitabu cha Warumi.Ndimi ndugu Charles Otunga,mwandaazi wa kipindi hiki ninayekuaga nikikutakia mibaraka na neema tele zake zake Mungu.Bwana akubariki na udumu katika neema yake.Kwaheri.